# OFISI YA RAIS - TAMISEMI .

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA.

Mob: 0752 924629, 0755313295, 0757 923133, 0753 929001.

SHULE YA SEKONDARI
MAKONGORO,
S.L.P 492,
BUNDA

KUMB. NA. MAKHS/STJ/JI/21 06/12/2019

JINA LA MWANAFUNZI ____________________
S.L.P 492,
BUNDA.

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MAKONGORO WILAYA YA BUNDA MKOA WA MARA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.**

1.0 Utangulizi.

Ninafurahi kukutaarifu kuwa umechanguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2020. Hongera sana.

Shule ya sekondari Makongoro iko umbali wa km. 2.5 Mashariki mwa mji mdogo wa Nyamuswa kandokando ya barabara kuu iendayo Mugumu-serengeti.

Shule hii ni ya kutwa inayo hostel kwa wasichana wenye nafasi chache kwa atayewahi (njoo upate maelekezo mapema iwezekanavyo). Masomo yanayofundishwa. Historia, jiografia, uraia,Kiswahili ,kiingereza,uhasibu,biashara, hisabati,baiolojia,fizikia na kemia. Masomo hayo yote yanafundishwa kwa lugha ya kiingereza isipokuwa somo la kiswahili tu.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 6/01/2020. Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe 6/01/2020 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 20/01/2019.

2.0. SARE:

**(a). Sare za shule.**

- Suruali mbili (2) nyeusi kwa mvulana zenye marinda (cerebration) mbili kila upande, mifuko miwili pembeni na mmoja nyuma upande wa kulia. Suruali isiwe modo.
- Sketi mbili (2) nyeusi kwa msichana zenye marinda yenye upana wa inchi 1.5 au sm 4. Mkanda wa sketi uwe na uapana was m. 6. Sketi iwe ndefu inayogusa kiatu. Waislam wanaruhusiwa kushona hijab nyeupe na bluu na sketi (sio suruali) zinazofanana na sare ya shule kwa kuzingatia maadili ya imani yao.

- Shati au blauzi mbili (2) nyeupe zenye mikono mifupi kwa wote.
- Soksi nyeupe jozi mbili (2) ndefu kwa wasichana zisizo na ulembo wowote ule na nyeusi kwa wavulana.
- Mkanda mweusi wa suruali kwa wavulana.
- Tai nyeusi zenye urefu usiovuka mkanda wa surualii au sketi. Pia ziwe na pini zake jozi mbili(2) kwa wote wavulana na wasichana.
- Jozi za viatu vyeusi vya ngozi vyenye kamba.
- Sweta ya Bluu yenye mikono mirefu, mshono wa (v) shingoni inayoruhusu kufunga tai,isiyokuwa na kola.
- T-shirt ya "darkblue" nzito yenye nembo ya shule na yenye kora.

<u>NB</u> : ***Mashati lazima yawe na nembo. Siku ya kuweka nembo itatangazwa kwa wanafunzi wote, gharama za kuweka nembo ni juu ya mzazi mwenyewe.***

**(b). <u>Sare za michezo.</u>**

- "Tracksuit" ya rangi ya bluu na viatu vya michezo (raba) kwa wote(viatu maalum vya michezo(njumu) kwa wavulana vinaruhusiwa) nguo hizi zitavaliwa siku ya michezo tu.
- Bukta na t-shirt ya bluu kwa wavulana tu kwa ajili ya mpira wa miguu.

3.0. <u>Vifaa vya shule.</u>

- ✓ Madaftari makubwa(counter quire 2) yasiyopungua 12.
- ✓ Mathematical set (bofa) 1.
- ✓ Kalamu za wino bluu/nyeusi ,penseli na ufuto za kutosha.
- ✓ Dictionary (English – English).
- ✓ Folder file kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zake Shuleni.
- ✓ Rula ndefu (cm 30).
- ✓ Karatasi za mazoezi ruled paper bando moja kwa kila mwanafunzi kwa ajili ya mazoezi. Mwanafunzi haruhusiwi kuchana daftari kwa ajili ya mazoezi (*NI MUHIMU SANA, ZINGATIA HILO*).

## 4.0. Vifaa vya usafi.

- Mfagio aina ya "chelewa na ndoo ndogo ya lita kumi kwa wote
- Jembe moja kwa wasichana
- Fyekeo moja kwa wavulana wote.

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE HII:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo ni muhimu kwako kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa nafasi hii. Ni ukweli usiopingika kwamba malezi ya wanafunzi kitaaluma kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya walimu na wazazi:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(b)

(c) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

(g) Kutunza mali binafsi, ya mtu mwingine na mali ya umma

(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote

(i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(j) Ni lazima kila mwanafunzi afahamu kuwa lugha ya kufundishia ni kingereza isipokuwa kwenye somo la Kiswahili tu. Muda wote wasiliana na walimu wako na wanafunzi wenzako kwa lugha ya kingereza tu.

(k) kila mwanafunzi anapaswa kuhudhulia baraza la shule,ukaguzi na usafi na kupandisha bendera ya taifa

(l) Mwanafunzi haruhusuwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (guest house).

(m) Ni marufuku kuendesha baiskeli ndani ya eneo la ukakamavu sshuleni. Eneo la ukakamavu linaanza geti kuu unapoingia shuleni na kuishia geti kuu unapotoka shuleni.

...E HEADMASTER
...KONGORO SECONDARY SCHOOL
...X 492 BUNDA
...ARA

(n) Ni marufuku kutembelea sehemu zifuatazo bila kibali maalumu na kazi rasmi:-

- Ofisi za shule
- Maabara
- Chumba cha walimu (staff room)
- Nyumba za wafanyakazi.

(n). Kila mwanafunzi anapaswa kuheshimu na kujali

- Wimbo wa taifa
- Nembo ya taifa
- Fedha za taifa
- Picha za viongozi wa taifa

(o) kila mwanafunzi aweze kuimba nyimbo zifuatazo kwa ufasaha na heshima.

- Wimbo wa taifa
- Wimbo wa Tanzania Tanzania nakupenda
- Wimbo wa shule

(p) Huruhusiwi kufuga ndevu,nywele na kucha

(q) Unapaswa kutunza mali za umma.

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE HII:

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria namba 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Hivyo ni muhimu kwako kumkumbusha mwanao ajue umuhimu wa nafasi hii. Ni ukweli usiopingika kwamba malezi ya wanafunzi kitaaluma kiroho na kimwili yanategemea ushirikiano kati ya walimu na wazazi:

(a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima

(b)

(c) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu

(d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

(e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule

(g) Kutunza mali binafsi, ya mtu mwingine na mali ya umma

(h) Kuvaa sare ya shule wakati wote

(i) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(j) Ni lazima kila mwanafunzi afahamu kuwa lugha ya kufundishia ni kingereza isipokuwa kwenye somo la Kiswahili tu. Muda wote wasiliana na walimu wako na wanafunzi wenzako kwa lugha ya kingereza tu.

(k) kila mwanafunzi anapaswa kuhudhulia baraza la shule,ukaguzi na usafi na kupandisha bendera ya taifa

(l) Mwanafunzi haruhusuwi kutembelea vilabu vya pombe, majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (guest house).

(m) Ni marufuku kuendesha baiskeli ndani ya eneo la ukakamavu sshuleni. Eneo la ukakamavu linaanza geti kuu unapoingia shuleni na kuishia geti kuu unapotoka shuleni.

HEADMASTER
SECONDARY SCHOOL
492 BUNDA

## 5.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE:

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile; uvutaji sigara, bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
5. Kupigana au kupiga au kutukana mwalimu, mfanyakazi au kiranja.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za starehe(**kama vile Baa,club n.k)**
10. Kupata au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu wengine
13. Kukataa adhabu kwa makusudi uliyopewa na mkuu wa shule, mwalimu au kiranja
14. Mwanafunzi kuwa na SIMU ya mkononi shuleni au kumiliki laini ya simu ama kifaa chochote kile kinachohusiana na simu.
15. Kutoroka shuleni.
16. Udanganyifu katika mitihani.
17. Kukwepa kufanya majaribio ya kila mwezi na mitihani yote.
18. Kutohudhuria masomo zaidi ya siku 90 bila taarifa au utoro
19. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua.
20. Matumizi ya lugha chafu kama kutukana, kukashifu.

**SHERIA/ KANUNI ZA SHULE ZISOMWE KWA MAKINI NA MWANAFUNZI NA KUZIELEWA KWA SABABU NDIZO ZINAZOLINDA AMANI NA UTULIVU SHULENI.**

**6.0 MENGINEYO:-**

- ✓ Fomu ya maelekezo ya daktari. Kila mwanafunzi ameambatanisha fomu maalumu inayotakiwa ijazwe na daktari kuhusu afya yake kufaa kuendelea na masomo au la. Fomu hii inatakiwa iwasilishwe siku ya kusajiliwa hapa shuleni. **AFYA YAKE IPIMWE KWENYE HOSPITALI YA SERIKALI YENYE VIPIMO VYOTE.**
- ✓ Kila mzazi/mlezi anatakiwa kujaza fomu na kusaini iwapo anakiri kukubali au kukataa nafasi aliyopewa mwanae. Aidha kushirikiana na uongozi katika maelekezo mengine yote yatakayotolewa na shule.

**HITIMISHO KWA WANAFUNZI:**

Nafasi uliyopewa ni mlango wa kuingia katika JAHAZI linalokuelekeza kwenye BANDARI ya mafanikio katika maisha.Inabidi uitumie nafasi hii kwa uangalifu ukiweka juhudi zako zote katika maelekezo utakayopewa hapa shuleni,iwe ndani ya darasa au nje.NIDHAMU, UTII na USHIKIRIANO ni mambo muhimu yatakayo kuwezesha kufikia mafanikio haya.Unatazamiwa kutafuta MAARIFA kukuza TAALUMA,kutunza MAZINGIRA na kuwa MTIIFU.Mwisho napenda kukutakia maandalizi mema ya kujiunga naShule ya Sekondari Makongoro.

**KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII.**

**M. A. GHATI.**
**MKUU WA SHULE.**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

MAKONGORO SEKONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 492,
**BUNDA.**

6/12/2019

The Medical Officer,
…………………………………………
…………………………………………
…………………………………………

**RE: ………………………………………………………….. (Full name of student)**

Please kindly examine the above, named as to his/her Physical and mental for enrolment as a student, the examination should include the following categories.

1. (a) Eye – sight (b) Hearing (c) Limbs (d) Speech (e) Venereal diseases (f) Leprosy (g) Epilepsy
2. Neurosis
3. Pregnancy
4. Other serious diseases

**THE HEADMASTER**

**PART B**

**MEDICAL CERTIFICATE**

(To be completed by a government Medical Officer)
I have examined the above named person and consider that he/she is physically FIT/UNFIT and mentally FIT/UNFIT or full time of schooling.

1. (a) Eye – sight ……………………………………………………………………
   (b) Hearing ………………………………………………………………………
   (c) Limbs …………………………………………………………………………
   (d) Speech …………………………………………………………………………
   (e) Venereal diseases …………………………………………………………
   (f) Leprosy ………………………………………………………………………
   (g) Epilepsy ………………………………………………………………………
2. Neurosis ……………………………………………………………………………
3. Pregnancy …………………………………………………………………………
4. Other serious diseases ………………………………………………………

Date: …………………………………………… Signature: ……………………………………

Station: …………………………………………… Designation: ……………………………………

## SHULE YA SEKONDARI MAKONGORO

## FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI: ________________________________

2. TAREHE YA KUZALIWA: ____________________

3. KABILA : ____________________

4. DINI: ______________________

5. SHULE ATOKAYO: ______________________________

6. MWANAFUNZI ANATOKA MTAA WA/ KIJIJI CHA ________________________

7. KATA YA: __________________ TARAFA YA: __________________

8. WILAYA YA: _________________ MKOA WA: ___________________

9. WAZAZI WOTE WAPO HAI.MMOJA YU-HAI/YATIMA (FUTA ISIYOHUSIKA)

10. JINA KAMILI MZAZI/MLEZI: ____________________________________

11. KAZI YA MZAZI/MLEZI: _____________ KAMA MLEZI TAJA UHUSIANO _________

12. ANUANI YA MZAZI/MLEZI:__________________SIMU: _________________

(a) Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.

(b) Nitahakikisha na ninaahidi kuhudhuria darasani siku zote za masomo.

(c) Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile pindi nikiwa mwanafunzi hapa Makongoro Sekondari. Naahidi nitadumisha nidhamu nzuri hapa shuleni.

(d) Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.

(e) Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakapoenda kinyume na sheria za shule.

______________________ ______________________

**JINA LA MWANAFUNZI** **TAREHE**

## FOMU YA AHADI YA MZAZI WA MWANAFUNZI

JINA LA MZAZI/MLEZI: ______________________________________________

(a) Nimesoma na kuyaelewa maelekezo na sheria za shule ya Sekondari Makongoro aliyopewa mwanangu na ninakubaliana nayo.

(b) Ninakubali nafasi aliyopewa mwanangu.

(c) Nitahakikisha kuwa mwanangu anapata mahitaji yake yote muhimu ya shule.

(d) Nitakuwa bega kwa bega na walimu katika kuhakikisha kuwa mwanangu anafuata sheria na kanuni zilizo shuleni. Nidhamu nzuri ya motto ndiyo mafanikio yake.

(e) Naahidi kuwa mwanangu hatashiriki mgomo, fujo na wala makosa ya jinai kama yeye mwenyewe alivyoahidi. Ikitokea akikiuka hatua kali za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yake.

______________________________ ______________________________

**SAHIHI YA MZAZI/MLEZI** **TAREHE**

______________________________________

**NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI**